TANGAZO LA SERIKALI NA. 67 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MSWISWI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Katika Eneo la Mswiswi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa Jumla na kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipakaifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MSW1 yenye majira-nukta 587760MS, 9031989KZ: baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KZ170˚28' kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MSW2 yenye majira-nukta 586556MS, 9032191KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KZ249˚35MG kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MS3 yenye majira-nukta 585748MS, 9030019KZ: baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KZ280˚29KS kwa umbali wa Kilomita 0.9 hadi kwenye alama ya upimaji namba MSW4 yenye majira-nukta 585919MS, 9029095KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ 03˚18'KS kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MSW5 yenye majira-nukta 586179MS, 9029110KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ 211˚21'MS kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MSW6 yenye majira-nukta 586768MS, 9029469KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ 68˚30'KS kwa umbali wa kilomita 2.7 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*